Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 81 No. 223 | SHAW.-DH.QAD 1442 AH | JUNI 2021 | IHSAN 1400 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Hakika Allah Hawadhulumu watu cho chote, lakini watu wanajidhulumu wenyewe. (Yunuus 10:45)

Maisha ya Mtume Mtukufu Muhammad saw

Yalivyosimuliwa na Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmud Ahmad r.a. Khalifatul Masih wa pili wa Masihi Aliyeahidiwa as

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

MASHITAKA YA MAKAFIRI WA MAKKA KWA ABU TWALIB NA UIMARA WA MTUME S.A.W.



Mafundisho haya yalipokuwa yakitolewa mara kwa mara kwa watu wa Makka, na mwelekeo wa watu wema kwenye Uislamu ukawa unaongezeka, basi siku moja wakuu wa Makka walijumuika na kwenda kwa baba yake mdogo, Abuu Twaalib na kumwambia: Wewe ni kiongozi wetu na ni kwa sababu yako wewe, sisi hatujamwambia chochote mwana wa nduguyo, Muhammad s.a.w.. Sasa wakati umefika ambapo wewe na sisi tuchukue uamuzi wa mwisho. Aidha wewe umfahamishe na umuulize kwamba hatimaye ni kitu gani anachokitaka kutoka kwetu. Kama aanataka kupata heshima, basi sisi tuko tayari kumfanya yeye awe mkuu wetu. Kama ni mwenye kutaka utajiri, basi kila mtu miongoni mwetu yu tayari kutoa sehemu ya mali yake kumpatia yeye. Kama tashi lake ni kuoa, basi atutajie jina la kila msichana wa Makka ampendae nasi tu tayari kumuozesha. Nasi hatutaki chochote toka kwake kama malipo na wala hatumzuii jambo lolote lile. Tukitakacho ni hiki tu kwamba aache kuisema vibaya miungu yetu. Bila shaka aseme kwamba Mungu ni Mmoja lakini asiseme kwamba miungu yetu ni mibaya. Kama atalikubali jambo letu hili dogo tu, basi tutakuwa na suluhu naye. Wewe umfahamishe na umfanye akubaliane na ushauri wetu huu, waila litakuwepo jambo moja kati ya mawili, aidha utalazimika kuachana na mwana (huyo) wa nduguyo au watu wako wataachana na wewe kwa kuukataa uongozi wako.

Jambo hili lilikuwa zito sana kwa Abu Twalib, kwani waarabu walikuwa na fedha kidogo tu. Furaha yao yote ilikuwemo ndani ya vyeo vyao. Viongozi walikuwa wakiishi kwa ajili ya watu wao na watu walikuwa wakiishi kwa ajili ya watu wao. Abuu Twaalib alifadhaishwa sana alipolisikia jambo hilo. Alimwitisha Mtume Muhammad s.a.w. na kusema: "Ewe mwana wa ndugu yangu! Watu wangu wamenijia na kunipa ujumbe huu na pamoja na hayo wameniambia pia kwamba kama mwana wa ndugu yako hataridhika na jambo lolote kati ya haya basi hapo tutakuwa tumeshamaliza kila njia ya uvumilivu, ikiwa hata hapo hataachana na njia yake, basi itakuwa ni jukumu lako kuachana naye na kama hauko tayari kuachana naye basi sisi tutaukataa uongozi wako na kuachana nawe.

Abuu Twaalib alipolisema jambo hili akawa anatokwa na machozi. Mtume s.a.w. alipoyaona machozi yake, naye pia akatokwa na machozi na kisha kumwambia: 'Ewe baba mdogo! Mimi sisemi kuwa utengane na watu wako na uambatane nami, wewe bila shaka achana nami na uungane na watu wako, lakini mimi naapa kwa Mungu Yule Mmoja Asiye na mshirika kwamba hata kama jua liletwe na kuwekwa kwenye mkono wangu wa kulia na mwezi uletwe na kuwekwa kwenye mkono wangu wa kushoto, siwezi kuacha kutoa mawaidha

Endelea uk. 3

Vijana wa KiAhmadiyya wafanya Ijtimaa yao ya 31



Mwaka huu, Ijtimaa ya Khuddamul Ahmadiyya Tanzania ilifanyika tarehe 18, hadi 20 Juni 2021 katika viunga vya Jumuiya huko Kitonga kata ya Msongola, Ilala, jijini Dar es salaam. Khuddam wakifanya ya 31 na Atfal ya 7. Ijtimaa ni kilele cha mwaka wa bidii na juhudi iliyoonyeshwa na mamia ya Khuddam na Atfal kote nchini. Lengo ni kuwaleta pamoja washiriki wetu wote wa Khuddam na Atfal katika onyesho la umoja katika utafutaji wa maarifa na uchamungu.

Kauli mbiu ya Ijtimaa ya mwaka huu ilikuwa "Salat". Hii pia ilikuwa lengo katika matukio yaliyo katika kalenda, na pia shughuli zingine

Endelea uk. 10

Siku ya Khilafat Jamia Ahmadiyya



Kwa msaada na Baraka za Allah wanachuo ,masheikh na waalimu wa Jamia Ahmadiyya waliadhimisha siku ya Ukhalifa katika siku ya Alhamisi ya tarehe 27/05/2021 mara baada ya sala ya adhuhuri.

Endelea uk. 10

Amir Jamaat ziarani kanda ya ziwa uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

KITABU NA HEKIMA

Binadamu ameenziwa na kupewa taadhima kubwa na Muumba wake. Kampa Uhuru wa kuchagua. Kampa uhuru wa kukubali au kukataa. Wataalamu wa dini tukufu ya Islam wanasema vilivyobaki vyote ni malaika – vinatii bila kubisha au kuuliza swali. Jua, mwezi, bahari, nyota, vyote hivyo vinatii tu. Hivyo inamuumiza sana binadamu ukimnyima uhuru wake wa kuchagua. Unanyakua haki aliyokabidhiwa na Allah. Fadhila nyingine aliyopewa binadamu ni akili. Anatumia akili zake kuamua. Anachekecha. Anatafakari. Anatizama pande mbili za sarafu. Halafu anafanya uamuzi.

Mafundisho ya Islam yamesimama katika msingi huo wa kumheshimu na kumuenzi binadamu. Islam inatambua uhuru wa mtu kukubali au kukataa. Na Islam inatoa heshima hiyo kwa sababu binadamu amepewa akili. Na ni jambo la kusikitisha wakati hazitumii akili na hapo ndipo linapokuja swali 'afalaa taakilun'. Kwa mantiki hiyo, Nabii Ibrahim a.s. anamuomba Allah apatikane Nabii atakayewafundisha watu Kitabu na Hekima. Kitabu hicho ni Quran tukufu na mfafanuzi wa hekima ni Mbora wa viumbe wote Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. Kila funzo la Islam limejengeka kwenye hekima na mantiki hadi akili inakubali kuwa jambo hili lina faida kimwili na kiroho. Islam kwa hiyo imekubalika kwa sababu ina hoja madhubuti na zenye faida. Waliodai kwamba Islam iliwalazimisha watu kuingia katika dini kwa upanga wameifanyia dhuluma kubwa kwani inaonyesha dhahiri shahir uhaba wao wa elimu kuhusu Islam na kutofungua kwao vitabu vya historia.

Ni hekima na mantiki vilivyowavuta watu na vinavyoendelea kuwavuta watu kuingia katika Islam. Wanafalsafa, washairi, na wasomi wa kila aina wamesumbuliwa sana na swali hivi kwa nini tumeumbwa? Kwanini tumekuja duniani? Shabaha ya kuja kwetu ni nini? Islam kwa kutumia mantiki inauliza, je tulikuja huku kwa hiyari yetu? Tulichagua kuja huku? Na je tunajua siku ya kuondoka? Kama hatujui, aliyetuleta, wala shabaha ya kutuleta tunawezaje kulijibu swali hili? Anayeweza kulijibu swali hii ni aliyetuleta. Aliyetutengeneza. Yeye tu ndiye anaweza kujua dhumuni na shabaha ya kutuleta. Atakuwa seremala wa ajabu, atengeneze kiti kizuri bila kufahamu kakitengeneza kwa nini na kwa shabaha ipi! Katu haiingii akilini. Islam inasema sisi tumeumbwa na Allah na yeye ndiye Anajua sababu ya kutuumba. Na yeye ndiye anayejua siku ya sisi kuondoka. Allah anasema sikuwaumba binadamu na jinni ila waniabudu. Tizama swali zito linavyojibiwa kwa mantiki na akili inaburudika na kukubali. Sala ya Kiislam inatoa fursa kwa siku watu kukutana msikitini kumwabudu Allah. Hapo wanapata fursa ya kufahamiana na kubadilishana mawazo. Na maendeleo yanakuja watu wanapokutana. Sala pia ni tiba ya mwili. Mazoezi ya mara kwa mara yanapunguza lehemu mwilini. Na lehemu inaleta matatizo ya moyo, kisukari na maradhi mengine mengi. Salat ni mazoezi yanayozuia hali ile ya kutosagika chakula vizuri (indigestion). Asubuhi tumbo linapokuwa tupu Mwislamu anatakiwa kusali rakaa ndogo lakini baada ya chakula cha usiku rakaa zinaongezeka. Tunasoma Takbira mwanzoni mwa sala tunanyanyua mikono yetu na mabega, kwa kufanya hivyo tunaongeza mtiririko wa damu. Akamat inafanya kazi hiyo pia. Kwenye sijida tunagusa chini na paji letu la uso, hii inaongeza damu safi kwenye bongo zetu. Moyo ni sehemu muhimu ya mwili. Inaeneza damu sehemu zote za mwili. Hata matendo yanayotendwa na mwili - simama, kaa ni mazoezi mazuri kwa moyo. Kuna hadithi ya Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. inayosema kuwa kiungo kimoja katika mwili kama ni kizima mwili wote utakuwa mzima, kikiwa kinaumwa mwili wote unaumwa. Kiungo hicho ni moyo. Akili itakataaje mafundisho mazuri kama haya.

Islam kama tulivyokwishaona inahimiza kukutana kwa watu. Kuna kukutana kila siku, siku ya Ijumaa, Iddi mbili na mkusanyiko wa dunia nzima ni Hija. Unafunga safari, unaacha kila kitu, unavaa shuka mbili, uwe mfalme au raia wa kawaida, hakuna mweusi au mweupe. Nyote kilio chenu ni LABEKA. Wapi unaweza kupata mkusanyiko wa binadamu wote kama unaofanyika katika mji Mtakatifu wa Makka ukiwa ni somo la vitendo kuhusu usawa wa binadamu? Na kuna kuchinja katika kumbukumbu ya tukio la Nabii Ibrahim a.s. aliyekuwa tayari kumtoa mwanae Ismail a.s. Na Islam inasema nyama na damu hivyo havimfikii Allah isipokuwa Uchamungu wenu. Hivyo katika kuchinja kuna somo ya kwamba tupeleke shingo zetu mbele tukitakiwa kufanya hivyo na Allah na ni ukumbusho ya kwamba kinachotakiwa kuchinjwa ni nafsi Amara, nafsi inayoamrisha kutenda mabaya. Na unapochinja mnyama mwingine asiwe karibu kuona anavyochinjwa mwingine. Kama Islam inaheshimu hisia za Wanyama, mtu anawezaje kusimama na kusema anatekeleza mauaji kwa ajili ya Islam? Ni uonevu mkubwa ambao safari hii hautoki nje bali ndani.

Somo jingine tunalolipata kutoka katika tukio hilo la Nabii Ibrahim a.s. ni kwamba lazima wanapo watu wa kujitoa muhanga kwa ajili ya furaha na maendeleo ya wengine. Sisi tunaposherehekea Iddi al adha ni kwamba aliyefanya tendo hili ni mwingine na sisi ndio tunaosherehekea. Watu wengine wanaumia ili wengine wafurahie. Tunaweza kukumbuka mateso waliyoyapata wapigania uhuru. Baadhi waliuwawa na wengine kujeruhiwa na leo tunaofaidika ni sisi. Ni utamaduni wa mshumaa kuwaka ukiisha wakati unatoa nuru.

Sote kwa pamoja tunao ulazima wa kuendelea kujifunza juu ya dini tukufu ya Islam. Dini hii ina mafunzo yanayoweza kutupa Jannatain – pepo mbili. Maombi yetu siku zote iwe – *Rabbi zidni ilman.*

Ziara ya Amir Jamaat Kanda ya Ziwa

Na **Mwl Abdullah H. Mbanga**

Amir wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya Tanzania, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry, mnamo mwezi Juni, 2021 alifanya ziara kubwa ya kuzunguka mikoa ya kanda ya ziwa kwa ajili ya kuhudhuria jalsa salana za mikoa hiyo. Ziara hiyo imekuwa ya kihistoria kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika mikutano hiyo, pia imeacha gumzo kutokana na mapokezi ya kiheshima yaliyofanywa na serikali kwa Amir wa Jamaat.

Akutana na IGP Sirro

Amir Sahib alitua katika uwanja wa Ndege wa Mwanza mnamo tarehe 16, Juni, yapata saa 1:45 asubuhi, kwa ndege ya shirika la ndege la taifa ATCL. Akiwa uwanja wa ndege, Amir Sahib alikutana na Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro. Viongozi hao walilakiana kwa bashasha ya hali ya juu, Amir na IGP walipata ya kufanya mazungumzo kwa muda wa dakika 15.

Katika mazungumzo hayo Amir Sahib alimweleza IGP Sirro madhumuni ya ziara yake na lengo la mikutano ya jalsa salana ambayo hufanywa na jamaat katika ngazi za mikao, taifa na hata kimataifa duniani kote, kwamba lengo kuu ni kufanya malezi kwa ajili ya waahmadiyya wapya na kuielimisha jamii kwa ujumla juu ya mafundisho ya Islam yanayosisitiza amani, upendo na maelewano baina ya watu. Kwa upande wake IGP alimshukuru jamaat kwa jitihada zake, pia aliipongeza Jamaat Ahmadiyya kwa hatua inazochukua katika kuhimiza amani nchini.

Kupitia mazungumzo hayo IGP Sirro alitoa wito kwa viongozi wa dini nchini kuwaelimisha waumini wao ya kuwa vurugu zinzofanywa kwa jina la dini huko kaskazini mwa Msumbiji na athari zake kuingia hadi kusini mwa Tanzania, kuwa si sehemu ya mafundisho ya Islam. Alisisitiza kuwa ni vyema waumini waelimishwe ya kwamba dini ya Mungu kamwe haikufundisha mauaji na uvunjifu wa amani. Amir Sahib alimwahidi IGP Sirro kwamba Jumuiya yake itaupa kipaumbele cha aina yake wito huo wa mkuu wa jeshi la Polisi nchini. Aidha, IGP alimkaribisha Amir Sahib ofisini kwake jijini Dodoma kwa moyo mkunjufu, baada ya Amir Sahib kuahidi kumtembelea kamanda huyo aliyekuwa akirejea Dodoma akitokea Mwanza alikokuwapo kwa ziara ya kikazi.



Amir na Mbashiri Mkuu pamoja na ujumbe wake katika picha ya pamoja na IGP Simon Sirro na maafisa wengine wa Jeshi la Polisi Tanzania walipokutana uwanja wa ndege Mwanza

Msindikizo wa Polisi

Amir sahib alipoagana na IGP, viongozi wa Jamaat Mkoa wa Mwanza walitumia nafasi hiyo kumuomba IGP msindikizo wa Polisi kwa ajili ya msafara wa Amir akiwa Mwanza. Kwa kuonesha heshima ya viongozi wa dini, IGP aliamuru mara moja gari la polisi lililomsindikiza yeye hadi uwanja wa ndege, liuongoze msafara wa Amir katika mizunguko yake yote mkoani humo.

Jambo hili halikufanyika jijini Mwanza tu, bali liliihusu misafara yote ya Amir Sahib katika kanda ya ziwa. Msafara huo uliokuwa na Magari madogo matano na basi moja, ulianza kuongozwa kwa heshima ya kipolisi kuanzia uwanja wa ndege wa Mwanza. Amir Sahib katika ziara hiyo aliungana na kundi la Masheikh kutoka mikoa mbalimbali nchini. Sheikh Abdul Rahman M. Ame, Katibu Mkuu wa ziada wa Jamaat Ahmadiyya nchini, Sheikh Nadeem (Dar), Sheikh Asif M. Butt (Morogoro), Sheikh Abid M Butt (Jamia), Sheikh Riaz A Dogar (Iringa), Sheikh Karimudin Shams (Mbeya), Sheikh Ihtisham (Mwanza) pamoja na Sheikh mkongwe mstaafu Yusuf A Kambaulaya aliyetokea Tabora ni miongoni mwa masheikh waliokuwamo katika msafara huo. Kadhalika kulikuwapo na wanajumuiya wapao 25 kutoka Dar, Dodoma na Singida waliosafiri hadi kanda ya ziwa kuhudhuria Jalsa hizo. Sadr Ansarullah, Bw. Ali Hamisi Mbambwa, Sadr Lajna Imaillah bi Zanana, nao ni miongoni mwa wanajumuiya waliokuwamo katika msafara. Msafara huo uliongozwa na magari ya Polisi katika kila Mkoa wa kanda ya ziwa. Hata katika vijiji vya mbali na miji msafara huo uliongzwa na sindikiza ya Polisi kwa usimamizi wa wakuu wa Polisi wa mikoa na wilaya husika. Kwa hakika ni ziara iliyoonyesha shani na heshima kubwa iliyo nayo jamaat katika nchi.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Maisha ya Mtume Mtukufu Muhammad saw

Kutoka uk. 1

ya Umoja wa Mwenyezi Mungu. Mimi nitaendelea kufanya kazi yangu hadi Mwenyezi Mungu Anipe umauti, wewe uyatafakari menyewe matashi yako.

Jibu hili lililojaa imani na khuluswi, lilitosha kuyafumbua macho ya Abuu Twaalib. Akafahamu kwamba; ingawa sikupata uwezo wa kuamini, lakini kupata uwezo wa kuiona imani hii ni utajiri mkubwa kuliko wote. Akasema, ewe mwana wa ndugu yangu! Nenda na uendelee kutekeleza wajibu wako. Kama watu wanataka kutengana nami, basi bila shaka watengane nami, lakini mimi siwezi kutengana nawe abadan. (Ibnu Hishaam na Zarqaani).

HIJRA (KUHAMA) KUELEKEA UHABESHI (ETHIOPIA)

Wakati dhulma ya watu wa Makka ilipofikia kiwango cha juu kabisa, basi siku moja Mtume Muhammad s.a.w. aliwaita wafuasi wake na kusema: Kuna ardhi fulani baada ya kuvuka bahari upande wa Magharibi, ambako dhulma haifanywi kwa sababu ya kumwabudu Mungu, watu hawauawi kwa sababu ya kubadili dini, huko kuna mfalme fulani muadilifu. Ninyi mfanye Hijra kwa kuhamia huko, huenda Mwenyezi Mungu Akajaalia njia ya urahisi kwa ajili yenu. Baadhi ya Waislamu, wanaume na wanawake, wakaenda zao Abbysinia (Ethiopia) kutokana na agizo lake hili.

Kuondoka Makka kwa watu hawa halikuwa jambo la kawaida. Watu wa Makka walikuwa wakijifahamu wao kuwa ndio waangalizi wa Kaaba. Yalikuwa ni majonzi yasiyovumilika kwa ajili yao kuihama Makka. Mtu aliyeweza kulifanya jambo hili ni yule tu ambaye hakuwa tena amebakiza sehemu yoyote duniani ya kujihifadhi. Kwa hiyo kuondoka kwa watu hawa lilikuwa ni tukio lenye kuumiza mno.

Halafu hata kuondoka kwa watu hao kulikuwa ni kwa kujiibia ibia (kwa siri kubwa), kwa sababu walikuwa wakifahamu kwamba kama watu wa Makka wakijua basi hawataturuhusu kuondoka na kutokana na sababu hii wakawa wanakosa hata fursa ya kuagana na ndugu na wapendwa wao. Hiyo ndio ilikuwa hali yao ya moyoni, hata wale waliowaona nao pia walisononeshwa na shida zilizowakumba.

Hivyo wakati msafara huo ulipokuwa ukitoka, Hadhrat Umar r.a. ambaye wakati huo alikuwa bado ni Kafiri na adui mkubwa wa Islam, akiwa ni mtu wa mstari wa mbele katika kuwasumbua Waislamu, akakutana, kwa bahati tu, na baadhi ya watu wa msafara huo, mmoja wao akiwa ni sahabiya fulani wa kike aliyeitwa ummu Abdillahi. Alipoona mizigo imefungashwa na wanyama wa kusafiria wakiwa tayari kwa safari, basi akafahamu kwamba watu hao wanaondoka na kuiacha Makka. Akasema: Ummu Abdillah, hii yaonekana kuwa ni mizigo ya wanaohama!

Ummu Abdillah anasema mimi nikamjibu: Naam, kwa haki ya Mwenyezi Mungu sisi tutaenda kwenye nchi nyingine kwa sababu ninyi mmetupa shida kubwa sana na mmetudhulumu mno na hatutarejea tena nchini kwetu hadi Mwenyezi Mungu Atujaalie sura ya wepesi na utulivu. Ummu Abdillah anasimulia kwamba Umar r.a. akajibu: Vizuri, Mungu awe pamoja nanyi, na nikaihisi simanzi ndani ya sauti yake ambayo kamwe sikuwahi kuihisi hapo kabla, kisha kwa haraka akaugeuza uso wake na kuondoka nami nikahisi kwamba tukio hili limemhuzunisha mno.

Watu wa Makka walipopata habari ya uhamaji wa watu hawa basi wakawafuatilia hadi wakafika baharini, lakini msafara ule wa Waislamu ukawa umeshavuka bahari na kuelekea Uhabeshi. Watu wa Makka walipofahamu hayo wakaamua kwamba utumwe ujumbe wa watu kwa mfalme wa Uhabeshi (Ethiopia) ili wamchochee dhidi ya Waislamu na kumshawishi awakabidhi Waislamu hao kwa watu wa Makka ili wawape adhabu ya kwa nini walidiriki kukimbia Makka kwa kushindwa kuvumilia dhulma (na mateso) ya viongozi wa mji wa Makka.

Katika ujumbe huo (wa watu wa Makka) alikuwemo pia Amru bin Al 'Aasw ambaye baadae alisilimu na nchi ya Misri ilitekwa chini ya uongozi wake wa kijeshi. Ujumbe huu ulienda Uhabeshi na kukutana na Mfalme na kuwachochea barabbara viongozi wa baraza la Mfalme, lakini Mwenyezi Mungu Akauimarisha moyo wa mfalme wa Uhabeshi na akakataa kuwakabidhi Waislamu kwa makafiri juu ya kushinikizwa sana na watu wale (Makafiri) na juu ya kushinikizwa na viongozi wa Baraza lake.

Ujumbe huu uliporejea bila mafanikio, watu wa Makka wakawaza hila nyingine ya kuwaita Waislamu hao nayo ni hii kwamba ienezwe habari hii kwa watu wa misafara ile iendayo Uhabeshi kwamba watu wote wa Makka wamekuwa Waislamu. Habari hii ilipofika Uhabeshi, basi Waislamu wengi wakarejea Makka kwa furaha, lakini walipowasili Makka wakatambua kuwa habari ile ilikuwa tu imeenezwa kwa utukutu na haikuwa na ukweli wowote ndani yake, hapo baadhi ya Waislamu wakarejea Uhabeshi na wengine wakabakia huko huko Makka. Miongoni mwa waliobakia Makka alikuwemo pia Uthman bin Madhw 'uun r.a. aliyekuwa mtoto wa kiongozi mmoja mkubwa wa huko Makka. Wakati huu alipewa hifadhi na Walid bin Mughira, aliyekuwa rafiki wa baba yake naye akaanza kuishi Makka kwa amani. Lakini kwa wakati huo akaona kwamba Waislamu wengine wanasumbuliwa na kufikishiwa mateso makubwa kabisa. Kwa kuwa alikuwa ni kijana mwenye ghera, alimwendea Walid na kumwambia; Mimi najiondoa katika hifadhi yako kwa sababu mimi siwezi kuona Waislamu wengine wakiteswa na mimi nikiishi kwa utulivu. Kwa hiyo Walid akatangaza kwamba sasa Uthman hayumo ndani ya hifadhi yangu.

Baada ya hapo, siku moja mshairi fulani maarufu wa kiarabu aliyeitwa Labid, alikuwa ameketi miongoni mwa wakuu fulani wa Makka akiwasomea mashairi yake na akasoma ubeti mmoja uliosomeka *Wa kullu na'iimin laa mahaalata zaailun* uliokuwa na maana ya; Hatimae kila neema ni yenye kufutika. Uthman akasema si sahihi, neema za Peponi ni za kudumu milele. Labid alikuwa ni mtu mkubwa sana, aliposikia jibu hilo akapandwa na hamaki na kusema: Enyi watu wa Quraish! Hapo kabla mgeni wenu hakuweza kudhalilishwa namna hii, sasa hii desturi mpya imeanza lini? Hapo mtu mmoja akasema; huyu ni mtu mmoja mpumbavu, usiyajali maneno yake. Hadhrat Uthman r.a. akaendelea kuyasisitiza maneno yake na kusema kuna jambo gani la upumbavu? Nimechosema ni kweli. Hapo mtu fulani akasimama na kumpiga ngumi ya nguvu sana usoni iliyosababisha jicho lake kutoka nje.

Wakati huo Waliid alikuwa ameketi katika kikao hicho. Kulikuwa na urafiki mkubwa kati yake na baba ya Uthman. Alihuzunishwa sana kuiona hali ile ya mtoto wa marehemu rafiki yake. Lakini kulingana na desturi za Makka, kwa kuwa Uthman hakuwa chini ya hifadhi yake, hivyo hakuweza hata kumhami. Kwa kuwa hakuweza kufanya lolote, hivyo akamwambia Uthman kwa uchungu: Ewe mwana wa ndugu yangu! Kwa haki ya Mwenyezi Mungu jicho lako hili lingeweza kusalimika na balaa hili wakati ulipokuwa ndani ya hifadhi madhubuti (yaani ulipokuwa ndani ya hifadhi yangu), lakini wewe mwenyewe uliiacha hifadhi hiyo na kuiona siku hii. Uthman akajibu, hicho kimechonikuta nilikitamani mwenyewe. Wewe walihuzunikia jicho langu hili limelopofuka, wakati jicho langu lililo zima lina hamu kubwa kwamba kwa nini halinitokei lililomtokea mwenzangu! Mfano wa Muhammad s.a.w. Mtume wa Mungu unatosha kwa ajili yangu, kama yeye anapata usumbufu, kwa nini mimi nisisumbuke? Ulinzi wa Mwenyezi Mungu unatosha kwa ajili yangu.

Itaendelea toleo lijalo

Amir wa Jumuiya Mkoani Geita

Na Mwl Abdullah H. Mbanga

Baada ya Amir Sahib kupokewa katika uwanja wa ndege wa Mwanza aliungana na ujumbe wake pamoja na wanajumuiya wengine kuelekea Nyegezi katika msikiti wa Baitul Kabeer yaliko Makao makuu ya kimkoa ya Jumuiya ya Ahmadiyya.

Baada ya kifungua kinywa, Msafara wa Amir Sahib ulishika njia kuelekea mkoani Geita. Msafara huo ulivuka kituo cha Busisi na hatimaye kuingia Sengerema, safari ilendelea hadi Geita mjini. Msafara ulifikia katika hoteli ya Lenny ambapo Amir Sahib na ujumbe wake walipumzika kwa muda mfupi, kabla ya kuelekea katika ofisi ya mkuu wa mkoa huo kwa ajili ya kukutana naye.

Mkuu wa Mkoa huo, Mh. Rosemary Staki, pamoja na kukutwa akiwa katika mkutano maalum, alipoombwa mlahaka na ujumbe wa Amir Sahib alisitisha kikao chake kwa muda ili akutane na viongozi wa Jamaat. Kikao baina ya Mkuu wa Mkoa na ujumbe wa Amir Sahib ulianza kwa Sheikh A. M. Ame kuwatambulisha wajumbe wa msafara huo kwa Mkuu wa Mkoa. Kisha Amir Sahib akamtambulisha Mkuu wa Mkoa juu ya Shughuli mbalimbali za Jamaat. Alielezea pia historia fupi ya harakati za Jamaat Ahmadiyya mkoani Geita, ambazo alisema, zilishika kasi si zaidi ya miaka 6 iliyopita. Alimwarifu Mkuu wa mkoa kuwa Jumuiya ina matawi yapatayo 20 mkoani geita, alimwalika mkuu huyo katika mkutano wa mwaka wa mkoa wa Geita ambao ungefanyika kesho yake katika Kijiji cha Nungwe, ambako pia ufunguzi wa msikiti ungefanyika. Hata hivyo kwa kuchelea nafasi ya Mkuu wa Mkoa, Amir Sahib alimsihi Mh. Staki kuhudhuria katika dhifa ya mlo wa usiku itakayoandaliwa

Endelea uk. 4

Amir wa Jumuiya Mkoani Geita

Kutoka uk. 3

kwa heshima yake katika hoteli ya Lenny.

Amir pia alimwelezea Mkuu huyo wa Mkoa uhusiano mwema uliopo baina ya Jumuiya na serikali zote zilizo madarakani katika nchi zote 210 duniani ambamo jumuiya imeenea. Alisema kuwa huu siyo msimamo wetu wa maneno tu bali tunalitekeleza hilo kwa vitendo bila kujali ni chama gani kilicho madarakani.

Naye Mkuu wa Geita katika hotuba yake aliukaribisha ugeni huo mkoani Geita na kuonyesha furaha yake kutokana na ziara hiyo. Alisema tunafurahi kuona kuwa katika mikoa mingi ya Tanzania mmeichagua Geita, hii kwetu ni faraja kubwa. Mkuu wa Mkoa pia alidhihirisha kufurahishwa kwake na msimamo wa Jumuiya wa kuwa na ushirikiano na Serikali. Alisema kuwa kuwa serikali inatamani kuona kuwa viongozi wake na wale wa dini wanazungumza lugha moja. Alisema kuwa anaamini kuwa ujio huo utaifanya jamii ya Geita kuwa ya watu wenye imani na uadilifu.



Amir na Mbashiri Mkuu pamoja na ujumbe wake walipomtembelea Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa Geita Bi. Rosemary Senyamule.

Hata hivyo Mkuu huyo wa mkoa aliomba radhi kwamba hatoweza kuhudhuria mkutanoni kutokana na ratiba yake kubanwa na mikutano, ingawa aliahidi kutuma mwakilishi wa ofisi yake.

Ufunguzi wa Msikiti Geita

Baada ya kikao na Mkuu wa Mkoa, msafara wa Amir Sahib ulianza safari kuelekea katika kijiji cha Kageye wilaya ya Geita vijijini ambako kulifanyika ufunguzi wa msikiti wa Jumuiya ya waislam waahmadiyya, Masjid Baitul Ilahi. Umati mkubwa watu uliupokea msafara wa Amir kwa takbir za shangwe. Msikiti ulifunguliwa kwa maombi ya kimya yaliyoongozwa na Amir na Mbashiri Mkuu, Sheikh T. A. Chaudhry.

Kisha hafla ikaanza kwa usomaji wa Kurani Tukufu iliyosomwa na Mwl Najat Fakim, Mwl Ali Tamim akasoma shairi. Baadaye rais wa tawi hilo akasoma risala ya tawi hilo, Bw. Musa Masalu, ambaye alielezea kwa ufupi historia ya kuingia kwa jamaat Ahmadiyya kijijini hapo. Aligusia pia shida ya mahala pa kuabudia ilivyowasumbua kutokana na eneo hilo kutokuwa na uislam kabla ya ujio wa jamaat Ahmadiyya. Pia risala ilitoa shukurani nyingi kwa jumuiya ilitolitatua tatizo hilo kwa kujenga msikiti mzuri wa kuvutia.

Katika hafla hiyo, walialikwa pia viongozi wa dini. Mchungaji wa Kanisa Katoliki na wa kanisa la AIC, katika salamu zao waliipongeza Jumuiya ya Ahmadiyya kwa jitihada zao za kuhakikisha watu wa maeneo hayo wanaachana na imani za kipagani.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho alionyesha kufurahishwa na ujenzi wa jengo la kupendeza uliofanywa na waahmadiyya katika kijiji chake. katika salamu zake alisema ujenzi wa jengo hilo la msikiti umekiinua kijiji chake kiasi cha kumfanya ajivunie kuwa historia hiyo imeandikwa wakati wa uongozi wake. Jengo la Msikiti wa Baitul Ilahi ndilo jengo bora zaidi katika kijiji hicho hadi sasa.

Mtendaji wa Kijiji cha Kageye, Mtendaji wa Kata ya Nyachiluluma na Katibu wa CCM wa kata hiyo, nao waliipongeza sana jamaat katika salam zao.

Akihutubia katika hafla hiyo, Sheikh Abdul Rahman Mohammed Ame, alielezea umuhimu wa kufanya ibada baada ya mtu kujiunga na jamaat Ahmadiyya. Alisisitiza kuwa wingi wa watu hauna maana yoyote katika dini iwapo hakuna ibada inayofanyika. Aliwataka waahmadiyya wapya waliojiunga katika eneo hilo kutambua umuhimu wa nguzo tano za dini na nguzo sita za imani na kuzitekeleza. Alirejea aya kadhaa za Kurani Tukufu ambamo imani na matendo mema zimetajwa kwa pamoja.

Baadaye Amir Sahib alitoa hotuba ya kufunga hafla hiyo iliyohudhuriwa na idadi kubwa ya watu wakiwamo akinamama na watoto kwa kutanabahisha kuwa thamani ya msikiti huo haitakuwapo iwapo watu hawatasimamisha sala. Amir sahib alisema kuwa msikiti huo ni nyumba ya Allah, hivyo pamoja kuwa wajenzi ni waahmadiyya, watu wa dini na madhehebu zote wanakaribishwa kumuabudu Mungu katika msikiti huo. Alitumia pia nafasi hiyo kuwakaribisha wanakijiji wote katika mkutano wa mwaka uliotarajiwa kufanyika katika kijiji cha Wigehe kesho yake. Hafla ilifungwa kwa maombi na baadaye dhifa ya chakula ilifuatia. Msafara wa Amir Sahib uliondoka majira ya jioni kurudi Geita mjini.

Dhifa ya Chakula na Mkuu wa Mkoa

Jioni ya tarehe 17, juni, 2021, Jumuiya ilimkaribisha mkuu wa mkoa wa Geita Mheshimiwa Rosemary Staki katika dhifa ya chakula cha usiku iliyofanyika katika hoteli ya Lenny mjini Geita. Mkuu wa mkoa alimbatana na mkuu wa wilaya ya Geita Mh Fadhili Mohammed Juma pamoja na maafisa wengine wakuu wa serikali ya mkoa.

Kabla ya dhifa zoezi la utambulishi lilirudiwa tena kwa faida ya mkuu wa wilaya, safari hii liliongozwa na Bw Yusuf Mgeleka, Rais wa Jamaat Ahmadiyya mkoa wa Shinyanga. Baadaye Amir Sahib alitoa maelezo mafupi ya kumshukuru Mkuu wa Mkoa kwa kuitikia wito walimpa asubuhi ya siku hiyo pamoja na kubanwa na shughuli nyingi.



Washiriki wa Jalsa Salana Geita

Baada ya chakula Mkuu wa Mkoa aliishukuru Jumuiya kwa mwaliko huo, aliomba pia wananchi waendelee Kumuombe Rais wa Nchi yetu Mh. Samia Suluhu Hassan. Lakini aliipokea kwa furaha zaidi kauli ya Amir Sahib ya kutaka kukifanya kijiji cha Kigeye kiwe modern (cha kisasa). Alisema anasubiri kwa hamu kubwa juu ya utimilifu wa jambo hilo hata kama litachukuwa muda mrefu. Aliomba Baraka kwa ajili ya msafara mzima na kuomba pia na mkoa wake uombewe Baraka. Dhifa ya chakula ilihitimishwa na neno la shukurani lililotolewa na Bw. Yusuf Mgeleka na hatimaye Amir Sahib aliongoza maombi ya kimya ambayo wahudhuriaji wote walishiriki.

Jalsa Salana Geita

Asubuhi ya tarehe 18, Juni, 2021, msafara wa Amir Sahib uliwasili kijiji cha Nungwe, kilichoko katika kata ya Nyamwililelwa, wilaya ya Geita vijijini. Mkutano ulianza sambamba na muda wa sala ya Ijumaa.

Zoezi la upandishaji wa bendera lilifanyika kabla ya ufunguzi wa mkutano, baadaye Mwl Ramadhani Mkiyeti alisoma Kurani Tukufu na kufuatiwa na Shairi lililosomwa na Nasiraat Ahmadiyya. Hotuba iliyofungua mkutano ilikuwa ni hotuba ya ijumaa iliyotolewa na Sheikh Abid Mahmood Butt kutoka Jamia Ahmadiyya Morogoro, ambayo ilizungumzia utii katika nidhamu ya ukhalifa. Baada ya sala hotuba ziliendelea kwa Sheikh Asif Butt kutoa hotuba juu ya kujitolea mali katika njia ya Allah, alielezea umuhimu na Baraka za kujitolea, pia alisisitiza juu ya kujitolea katika kazi za jamaat na kuwatoa watoto wakfu kwa ajili ya kuhudumia dini. Mada ya tatu ilihusu malezi. Sheikh Abdul Rahman Ame alielezea kuhusu utekelezaji wa ibada mbalimbali na namna ya kupata uchamungu baada ya kujiunga na jamaat. Sheikh Karimudin Shams alitoa hotuba juu ya imani za msingi za Jamaat Ahmadiyya na kuelezea tofauti iliyopo baina ya jamaat na madhehebu nyingine za kidini. Katika hotuba yake alisisitiza pia juu ya utii wa sheria za nchi.

Baadaye zilifuata salamu za wageni waalikwa ambapo Mtendaji wa kata ya Nyamwiholelwa, Bw Simoni Maduka Joseph, Mtendaji wa Kijiji cha Nungwe, Bw. Elikana Jackob Ncheye, Mwenyekiti wa Kijiji Bw. Revocatus Matale na Katibu wa CCM kata hiyo Bw. Mateso Meleka walitoa salamu kwa nyakati tofauti. Katika salamu zao waliipongeza na kuishukuru Jamaat kwa kuleta mkutano Mkubwa wa aina hiyo katika eneo lao. Waliahidi pia kutoa ushirikiano wa kila hali kwa jamaat Ahmadiyya na kwamba wakiwa kama viongozi wa serikali, watahakikisha kwamba shughuli za jamaat zinafanyika kwa amani bila bughudha yoyote. Mwishowe Amir Sahib alitoa hotuba ya kufunga mkutano. Aliwashukuru wote waliohudhuria katika jalsa hiyo na kuwatakia safari njema za kurudi makwao. Lakini pia aliwasisitiza kuyazingatia yote yaliyoelezwa katika hotuba mbalimbali na hatimaye kuongoza maombi ya pamoja kurasimisha ufungaji wa mkutano. Taarifa zilionyesha kuwa watu 1268 walihudhuria mkutano huo.

Jalsa Salana Simiyu

Na **Mwl Abdullah H. Mbanga**

Msafara wa Amir Sahib ulitoka ulifika simiyu wakati wa Magharibi, tarehe 20, juni, 2021, msafara ulipokewa mjini Bariadi na wanajumuiya wachache wa mjini wakiongozwa na Mbashiri wa Mkoa huo, Sheikh Ali Dino Tahir. Sala ya Magaharibi na Ishaa ilisaliwa katika hoteli ya Sunga, mjini Bariadi ambapo msafara huo ulifikia. Asubuhi iliyofuata msafara wa kuelekea wilayani Itilima ulianza. Njiani Amir Sahib alikagua kiwanja cha jamaat katika eneo la Gangabili ambacho ni kikubwa kinachotosha kujenga msikiti, nyumba ya Mbashiri na huduma nyingine kama shule au zahanati.

Msafara ulifika Itilima yapata saa 4:00 asubuhi, amir Sahib alipata wasaa wa kukagua eneo la jalsa Gah, jikoni pamoja na maeneo mengine. Mkutano ulianza majira ya saa 5:00 kwa usomaji wa Kurani Tukufu uliofanywa na Mwl Idrissa Saguda, ambaye katika namna ya kuvuyia zaidi alitoa tafsiri ya Kiswahili nay a kisukuma. Mwl Mustafa Habib, alisoma shairi.

Amir Sahib aliyekuwa ndiye mwanyakiti katika vika vyote vya Jalsa za kanda ya ziwa alisimama na kutoa hotuba ya ufunguzi wa mkutano huo. Katika hotuba yake aliendelea kusisitiza juu ya kuwaombea na kuwatii viongozi wakuu wa kitaifa, wa kimikoa na kiwilaya, na hata viongozi wadogo wa mitaa. Alihamasisha juu ya kuwaunga mkono, kuwasaidia na kuwaombea viongozi wa nchi. Alisema kuwa kutokana na Jumuiya ya Ahmadiyya kutambua umuhimu wa viongozi hao ndiyo maana imekuwa ikiwaalika katika mikutano yake yote na kwamba imekuwa karibu mno na viongozi wa serikali katika kila ngazi. Pia aliwataka waahmadiyya pamoja na wananchi wengine kuishi kwa kutii sheria za nchi kwa kuwa hayo ni maagizo ya Allah na Mtume wake Muhammad saw.

Hotuba ya kwanza ilitolewa na Sheikh Abid Mahmood aliyeendelea na mada ileile ya utii katika nidhamu ya ukhalifa. Baadaye sheikh Asif Butt alitoa hotuba juu ya umuhimu wa kujitolea mali katika njia ya Allah. Katika hotuba yake aliwapongeza wanajumuiya wa Simiyu ambao walichangia kiasi kikubwa cha gharama za chakula katika mkutano huo. Hata hivyo aliwasisitiza kuendeleza tabia ya kutoa katika njia ya Allah, kwa kuwa ni kupitia michango hiyo ndipo jumuiya ya Allah inaweza kuleta maendeleo katika nyanja za kiroho.

Baada ya hotuba hiyo kukafuata salamu za wageni waalikwa ambapo viongozi mbalimbali wa serikali na wale wa kijamii walielezea kufurahishwa kwao kwa kukaribishwa katika mkutano huo. Waliipongeza Jamaat Ahmadiyya kwa ushirikiano inaouonyesha katika mambo mbalimbali ya kijamii na kiserikali. Baadhi ya waahmadiyya wapya pia walieleza hisia zao kutokana na ujio wa viongozi wakuu wa jamaat katika eneo hilo.



Mkutano huo ulifungwa kwa hotuba ya Amir Sahib aliyeelezea umuhimu wa watu kufanya mabadiliko ya kweli ya kikhulka baada ya kujiunga na jamaat. Alisema kwamba ili mtu awe ahmadiyya wa kweli ni lazima aachane na desturi zote chafu alizokuwa nazo kabla. Alisisitiza kwamba imani na matendo mema ndiyo kauli mbiu rasmi ya mikutano yote ya kanda ya ziwa kwa mwaka huu. Amir Sahib alifunga kikao kwa kuongoza maombi ya pamoja.

Baadaye sala ya Adhuhuri na Alasiri zilisaliwa katika eneo la Jalsa Gah chini ya uongozi wa Amir Sahib. Kisha chakula cha mchana kilihudumiwa kwa washiriki wote. Msafara wa Amir Sahib uliondoka Itilima kunako saa 1:30 na kuelekea katika eneo la Gangabilili ambapo Amir Sahib aliweka jiwe la msingi la msikiti katika kiwanja cha Jamaat. Baada ya hapo watu walitawanyika na kuhitimisha ziara ya Amir Sahib katika Kanda ya Ziwa.

Jalsa Salana Shinyanga

Na **Mwl Abdullah H. Mbanga**

Msafara wa Amir Sahib ulifika Shinyanga majira ya 6:30, mchana na kulakiwa kwa Takbir nyingi. Kundi kubwa la waandishi wa habari lilikuwapo katika uwanja wa mkutano uliokuwa mkabala na msikiti wa Baitul Muqeet, katika eneo la Wigehe mjini Kahama, makao makuu ya jamaat katika mkoa wa Shinyanga.

Baada ya mapumziko mafupi, Amir Sahib alifanya mahojiano na waandishi wa habari katika ukumbi wa Mission House. Waandishi kutoka TBC, ITV na Radio One, Star TV na RFA, magazeti kama Nipashe, Mwananchi na wawakilishi wa blog mbalimbali za mitandaoni. Baada ya mapumziko Mafupi, Amir Sahib aliongoza sala ya adhuhuri na alasiri katika Jalsa Gah. Baada ya sala chakula cha mchana kikao cha jalsa kilianza chini ya uenyekiti wa Amir Sahib. Kurani Tukufu ilisomwa na Mwl Idi Shabani, baadaye usomaji wa shairi ulifanywa na Khudamul Ahmadiyya.

Hotuba ya kwanza ilitolewa na Sheikh Karimudin Shams wa Mbeya, ambaye alifafanua juu ya imani za waahmadiyya.

Hotuba ya pili ilitolewa na Sheikh Yusuf Athumani Kambaulaya ambaye alifafanua juu ya wajibu wa kila mwahmadiyya. Hotuba ya tatu ilitolewa na Sheikh Riaz Ahmad Dogar wa Iringa. Yeye alitoa mada juu ya malezi ya watoto.

Sadr Ansarullah, Bw Ali H. Mbambwa naye pia alipata nafasi ya kuhutubia katika mkutano huo. Katika hotuba yake fupi alielezea dhana nzima ya tanzim katika Jamaat, alizitambulisha tanzim za Ansarullah kwa ajili ya watu wazima, Khudamul Ahmadiya na Atfalul Ahmadiyya kwa ajili ya vijana na watoto wa kiume, na pia Lajna Imaillah na Nasiraatul Ahmadiyya kwa ajili ya akinamama na mabinti. Alieleza pia malengo ya kuasisiwa kwa tanzimu hizo kwamba ni kuisaidia jamaat katika mambo ya msingi ya kuasisiwa kwa jamaat. Pia Sadr Sahib katika Hotuba yake aliwaomba walimu na Masheikh wa Jamaat wa kanda ya ziwa kutoa ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa masuala ya kitanzim bila kujali marika yao. Alisema wao kama walimu ni wataalam wa mambo mengi, hivyo msaada wao unahitajika sana katika tanzimu za eneo hilo ambao wengi wa wanachama wake ni wanajumuiya wapya.

Katika mkutano huo, alihudhuria pia naibu Katibu Mkuu wa CCM wilaya ya Kahama bw. Harun, ambaye naye alipewa nafasi ya kuzungumza. Mwishoni mwa hotuba yake fupi aliahidi kwa niaba ya chama na serikali kinayoiongoza kwamba kitatoa ushirikiano wa kila namna kwa Jamaat Ahmadiyya katika shughuli zake za uenezi wa amani na kwamba serikali ipo tayari kwa msaada wowote iwapo utahitajika.

Mkutano huo ulifungwa na Amir Sahib ambaye alitoa hotuba fupi ya kufunga mkutano. Katika hotuba yake aliwaasa wanajamaat na watu wengine kutumia muda uliobaki wa maisha yao katika kumwelekea Allah. Alitoa wito wa kuwatii na kuwaombea viongozi wa serikali ambayo inatoa uhuru wa kuabudu kwa watu wake. Katika hotuba hiyo pia alikemea juu ya watu wanaotumia dini kuanzisha vurugu au kushawishi uasi juu ya serikali. Alisema kuwa dini inafundisha amani na upendo na kwamba ni kauli mbiu ya jamaat Ahmadiyya ya kuwa *Upendo kwa wote bila chuki kwa yeyote*. Amir Sahib alifunga mkutano saa 12:00 kwa kuongoza maombi. Baada ya sala ya Magharibi na Ishaa na Chakula cha usiku, kipindi cha maswali na majibu kilifanyika kikiongozwa na Masheikh A. M. Ame, Karimudin Shams, Abid Mahmood na Asif Butt. Kipindi hicho kilitamatishwa mnamo saa 3:00 usiku.

Mkutano na waandishi

Juni 20, 2021, ratiba ilianza kwa mkutano wa Amir na waandishi wa habari uliofanyika katika ukumbi wa Mission House hapo Wigehe. Mkutano huo ulianza saa 2:30 na kuhitimishwa mnamo sa 3:15. Mkutano ulianza kwa Amir Sahib kutoa utambulisho wa Jamaat Ahmadiyya. Alieleza historia fupi ya jamaat na muasisi wake. Aidha alieleza juu ya uenezi wa Jamaat duniani na hatimaye kueleza juu ya harakati za jamaat mkoani Shinyanga.

Alidokeza kuwa jamaat Ahmadiyya Mkoani Shinyanga ina matawi yapatayo 50 yenye uongozi kamili, na matawi 15 ambayo bado ni machanga. Miongoni mwa matawi hayo alisema kuwa matawi 21 tayari yana misikiti na nyumba za walimu. Pia aligusia juu ya miradi ya maji na umeme wa jua inayoendeshwa na jamaat katika vijiji mbalimbali mkoani humo.

Baadaye Sheikh Ame Sahib, ambaye alikuwa akifasiri maelezo ya Amir katika Kiswahili, aliongeza kwamba jamaat hii iliingia Tanzania mwanzoni mwa karne ya 20 na kupata usajili mnamo mwaka 1934. Sheikh Ame aliwaambia waandishi kuwa Jamaat inajihusisha na shughuli za kidini tu pasipo kuingilia harakati zozote za kisiasa au kuwania madaraka ya dola. Alifafanua pia kwamba Jumuiya hii haiungi mkono kwa vyovyote masuala ya ugaidi unaohusishwa na dini na kusema kuwa dhana hiyo si miongoni mwa mafundisho ya Islam.

Akitaja jambo lililoisukuma jamaat Ahmadiyya kuanza harakati maalum za mahubiri mkoani Shinyanga, alisema kuwa ni wimbi la mauaji ya vikokngwe lililotokana na imani za kishirikina. Kwa hali hii jamaat iliamua kuleta mahubiri yake ili kuwatoa watu katika imani hizo potofu, jambo ambalo alisema limefanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Baadaye maswali ya waandishi yalifuata, wengi wao waliuliza juu ya miradi ya maji inayoiendeshwa na jamaat katika mkoa huo. Baadhi yao walitaka kujua msimamo wa jamaat kuhusiana na siasa za nchi. Wapo pia walioiuliza juu ya uwezekano wa jamaat kuwekeza katika huduma za kijamii mkoani humo.

Bustani ya Washairi

MWALIMU TUTAONANA

1. Ndiye wetu Subhana, Aliyeumba dunia
Usiku pia mchana, vipo mwezi nyota jua
Muongozo bora sana, akaja kutuwekea
Atapopenda Jalia, mwalimu tutaonana

2. Mwalimu tutaonana, atapopenda Jalia
Kitonga unatuhama, Kibiti waelekea
Uwende kwa usalama, kaongoze yarabia
Atapopenda Jalia, mwalimu tutaonana

3. Pazuri ulisimama, mazuri kuelezea
Ili tuwe waja wema, tufanye yenye kufaa
Mara nyingi alisema, ukumbusho kutugea
Atapopenda Jalia, mwalimu tutaonana

4. Elimisho ulinena, hukuchoka kurudia
Kama vile saming'ina, kutii na kusikia
Asiye taka kupona, mbele asije jutia
Atapopenda Jalia, mwalimu tutaonana

5. Sasa ifungue tena, kuraani yetu njia
Sura ya kumi na nane, jaribu kuipitia
Aya ile utaona, hamsini na nane tua
Atapopenda Jalia, mwalimu tutaonana

6. Twakumbuka mengi sana, yasoisha elezea
Mapoli yalishehena, hakuna pa kupitia
Mbawala alipambana, Mola atakulipia
Atapopenda Jalia, mwalimu tutaonana

7. Sote tulishikamana, kung'aa jalsa ghaa
Tulizichukua zana, kuanza kujitolea
Khuddamu nao lajna, wale ansarullah
Atapopenda Jalia, mwalimu tutaonana

8. Lile shimo la upana, chemba alisimamia
Paka vyoo kujazana,nguvu zake alitia
Mjalie maulana, Baraka kumjazia
Atapopenda Jalia, mwalimu tutaonana

9. Mariamu luambana, mengi ulivumilia
Kina mama wasichana, kama tulikukwazia
Imefika twaachana, safari njema ombea
Atapopenda Jalia, mwalimu tutaonana

10. Ni mambo ya kiungwana, yale tulokutendea
Nakama tulikosana, twakuomba msamaa
Usahihi kupendana, mtume katuambia
Atapopenda Jalia, mwalimu tutaonana

11. Jambo hili kuagana, simanzi kapelekea
Mabibi ata mabwana, yabidi kulizoea
Pwani sio kama Ghana, tumaini twajigea
Atapopenda Jalia, mwalimu tutaonana

12. Namshukuru Rabana, hakika kasaidia
Muda huu wa mchana, shairi kujitungia
Afya ni kitu mwanana, sina budi shukuria
Atapopenda Jalia, mwalimu tutaonana

CHUMA CHIKOLI MOTO:

1.Ndugu zangu waungwana, mambo yamebadilika
Huna haja ya kununa, acha mbwembwe chakalika
Laa sivyo utaona, machozi yanakutoka
Embu twende na upepo, tusije kupoteana.

2. Tusije kupoteana, yakazuka makelele
Tupunguze kujichana, tusisahau tembele
Nimefikiria sana, nimeangalia mbele
Embu twende na upepo, tusije kupoteana.

3. Usishangae kwa nini, nimeamua kunena
Hizo siku za usoni, watu watakataana
Hawatakwenda chooni, tumboni kitu hakuna
Embu twende na upepo, tusije kupoteana.

4. Embu tujibane sana, tujisogeze golini
Vya kunoga basi tena, hatupiti hotelini
Hali tete waungwana, tukimbilie mbinguni
Embu twende na upepo, tusije kupoteana.

5. Hakuna kuku maini, ni majanga kila kona
Mambo sio majumbani, na Uchumi unabana
Lazima tuwe makini, maisha ya kulingana
Embu twende na upepo, tusije kupoteana.

6. Januari naiona, Ada kubwa mashuleni
Kama inawezekana, msomeshe mtaani
Tuacheni kujivuna, anasoma ushuani
Embu twende na upepo, tusije kupoteana.

7. Kodi ya nyumba jamani, mwenyewe ameshanuna
Kila siku mlangoni, wala Amani hakuna
Ukiwapo duniani, jitahidi kupigana
Embu twende na upepo, tusije kupoteana.

8. Ngoja ikushike homa, tena homa kweli kweli
Mara umeme kuzima, uje uone kejeli
Njaa nayo inauma, huna hata Mia mbili
Asilaumiwe mtu, tuendako ndo kwenyewe.

9. LUKU iko ukingoni, maji bombani hakuna
Kila kukicha wageni, wanapenda vya kunona
Kilio cha ukubwani, umebanwa kila kona
Asilaumiwe mtu, tuendako ndo kwenyewe.

10. Tuliyajua mapema, pia tulikumbushana
Wala hakuna kuhama, na kesi pia hakuna
Ukibisha utakwama, usijifanye kijana
Asilaumiwe mtu, tuendako ndo kwenyewe.

11. Nguo mpya kwetu mwiko, fanya mambo ya maana
Pilau ya mualiko, kwako jiko limenuna
Sikumbuke diko diko, zama za hivyo hakuna
Asilaumiwe mtu, tuendako ndo kwenyewe.

12. Hatuazimani hela, kuhofia kugombana
Kila mtu hana hela, si Mzee si Kijana
Hakuna picha ni trela, muigizaji mchina
Asilaumiwe mtu, tuendako ndo kwenyewe.

13. Fanya kazi tofauti, watoto wasile nyasi
Tembeza hata mashati, uza hata mananasi
Usifanye kwa shuruti, usije toka kamasi
Asilaumiwe mtu, tuendako ndo kwenyewe.

14. Muda umeshawadia, tujifungeni mikanda
Hapana kulia lia, tujifanyeni manunda
Ndugu ninawausia, tujiandae kukonda
Asilaumiwe mtu, tuendako ndo kwenyewe.

15. Ngoja niishie hapa, nisije vuka mipaka
Lawama msijenipa, kwamba sikuwakumbuka
Mimi ni wa hapa hapa, sikubali kuumbuka
Asilaumiwe mtu, tuendako ndo kwenyewe.

Abdallah Kalindima (K-mtoto)
#Mmakonde Msomi

KUMBUKIZI SISIMUZI

Zile sala sisimuzi, Zenye kwikwi na vilio
Zisimikazo mizizi, Kwazo hupandishwa vyeo
Zimebaki simulizi, Hotuba na marejeo
Tumepoteza kiini, Maganda kufurahia

Na siye wa ndoto moja, milele kufurahia
Njoo uone kihoja, Ijapo ya kutimia
Twakusanyika pamoja, Dunia Kusimulia
Tumepoteza kiini, Maganda kufurahia

Wale tuso na majina, Wanijua Mimi nani?
Tujijuao mapana, Mie uzao Fulani
Kazi ipi umefana, Huonekani safuni
Tumepoteza kiini, Maganda kufurahia

Wale wa kati kwa kati, Upo dinini uhuni?
Kote kote huwapati, So mbinguni ardhini
Wano jivika mashati, Viduku, rasta vichwani
Tumepoteza kiini, Maganda kufurahia

Haya nasi watumishi, waterezesha kondoo
Uchao malalamishi, vya kuonewa vilio
Tumetupa utumishi, mebaki visingizio
Tumepoteza kiini, Maganda kufurahia

Twasimulia wa kale, Wacha Mungu na watawa
Tumekufa kwa mishale, kuzileka nyengo sawa
Hatutofuzu milele, kama twajiona sawa
Tumepoteza kiini, Maganda kufurahia

Shunda Mshundia Wana
Daluni, Tanga

MASHEIKH WAANDISHI

Hodi kwako mhariri, gazetini nimefika
Naomba hii habari, gazetini kuiweka
Waisome Ikwiriri, Tabora hadi Nguruka
Ee Mola Wabariki, Masheikh Waandishi

Tumebaki na athari, kwa yale waloandika
Elimu yao Johari, kila mara yamulika
Twakuomba ya kahari, tuzidi kufaidika
Ee Mola Wabariki, Masheikh Waandishi

Kwanza alotafsiri, Kurani kwa hakika
Alikuwa mwenye ari, Sheikh wetu Mubaraka
Pia Sheikh Munawari, kalamuye iliwaka
Ee Mola Wabariki, Masheikh Waandishi

Na mwengine mwenye ari, ni Jamil msifika
Anaweza ushairi, na vitabu kuandika
Ni Sheikh alo mahiri, majibu akiandika
Ee Mola Wabariki, Masheikh Waandishi

Durran namkariri, ni simba wa kuandika
Muda wake sio siri, mengi aliyaandika
Na leo tunanawiri, maandiko tukishika
Ee Mola Wabariki, Masheikh Waandishi

Kwa uandishi mahiri, Jumuiya nivutika
Uongofu tafsiri, Kaluta aloandika
Nikafungukiwa siri, Masihi ni wa Rabuka
Ee Mola Wabariki, Masheikh Waandishi

Pia mno tafsiri, Masihi aloandika
Na Mola awasitiri, Awape ya kutukuka
Nasi tupate athari, tusome kwa uhakika
Ee Mola Wabariki, Masheikh Waandishi

Watadumu sio siri, Swahili napokutika
Jumuiya ikidhihiri, watu wakajumuika
Kazi yao kidhahiri, ndio njia yamulika
Ee Mola Wabariki, Masheikh Waandishi

Hassan Sango (Jange Muqaddas kwenye karatasi)

KIFO.

HU! Japo kina umiza, Ndo hivyo hakikwepeki,
Chabaki kutushangaza, Wala hakitabiriki,
Mioyoni hudumaza, Kifo hakiombeleki,
Dah! Kifo cha huzunisha, Pia na kusikitisha.

Jamani inaumiza, Pindi kinaposikika,
Twa baki twa jiuliza, Kama kina epukika,
Kifo cha tujaliliza, Hofu na kuweweseka,
Mmmh! Kifo cha huzunisha, Kifo kifo tusamehe.

Nacho pia kiliumbwa, Kwa kutumaliza sisi,
Watu wote tutakumbwa, Kutengana zetu nafsi,
Ardhi nyingi zitachmbwa, Na tutaingizwa sisi,
Tena kweli kifo kipo, Hakuna kujidanganya.

Lo! Kifo hakibagui, Si mkubwa si mtoto,
Umbile hakichagui, Kipo hata kwenye joto,
Kinapokuja hujui, Kifo kama ka la moto,
Kifo hakina huruma, Yeyote cha Mchukua.

Cha sababishwa kwa mengi, Ajali magonjwa pia,
Tena cha ondoa wengi, Wabakiao walia,
Na cha sababisha mengi, Maumivu kutwachia,
Kifo si tumeumbiwa, Twa subiri chukuliwa

Abubakary Abdallah Mwita
Mkurya halisi.

MPATIE ZURI FUNGU

1. Ya Rabi Mola Karima, haya yote ni ya Mungu
Wewe ndiye Mwenye dhima, Muumba ardhi na mbingu
Tunakula vya kuchuma, kwenye wetu ulimwengu
Mpatie zuri fungu, Issa wa Mwakitalima

2. Issa wa Mwakitalima, mpatie zuri fungu
Alikuwa mja mwema, sio mtu wa majungu
Mapungufu yapo kama, jalali fungua pingu
Mpatie zuri fungu, Issa wa Mwakitalima

3. Watu tulishika tama, sikutuliona chungu
Muda wa mchana mwema, tulipokea machungu
Tiba zote ziligoma, alimchukua Mungu
Mpatie zuri fungu, Issa wa Mwakitalima

4. Alikuwa mkarima, haya mimi sio yangu
Majirani walisema, tena mazuri mafungu
Walizijaza heshima, mweusi sio mzungu
Mpatie zuri fungu, Issa wa Mwakitalima

5. Sifadhe hazikukoma, nyingi kama sungu sungu
Ana utu na huruma, wala sio nungunungu
Maneno waliyatema, ni matamu si machungu
Mpatie zuri fungu, Issa wa Mwakitalima

6. Msiba umetuchoma, sisi jamaa na ndugu
Dada Naomi Amina,tuyakumbuke ya tangu
Sharti la tano soma, tuujaze uchamungu
Mpatie zuri fungu, Issa wa Mwakitalima.

Rehema Fadhili
Kitonga, Dar es salaam

Zebaki na Mchanja Kuni

Mchanja kuni alikuwa akikata mti ukingoni mwa mto, wakati shoka lake, akiangaza kutoka kwenye shina, shoka lake likamponyoka na kuangukia ndani ya maji. Alipokuwa amesimama kando ya maji akiomboleza kupotelewa kwake, Zebaki alitokea na kumuuliza sababu ya huzuni yake; na baada ya kujua kilichotokea, kwa huruma ya shida yake, akaingia ndani ya mto na, akaleta shoka la dhahabu, akamwuliza ikiwa ndilo lile alilolipoteza. Mchanja kuni huyo alijibu kwamba siyo, na Zebaki kisha akazama mara ya pili na, akaleta shoka la fedha, akauliza ikiwa hiyo ilikuwa yake. "Hapana, hilo pia sio langu," alisema yule mchanja kuni. Kwa mara nyingine Zebaki alizama ndani ya mto, na akaleta shoka iliyopotea. Mchanja kuni alifurahi sana kupata mali yake, na alimshukuru mfadhili wake kwa uchangamfu; na mfadhili alifurahishwa na uaminifu wake hata akamtengenezea zawadi ya mashoka mengine mawili.



Mchanja kuni alipowaambia wenzie hadithi hiyo, mmoja wao alipatwa na wivu wakaamua kujaribu bahati yake mwenyewe. Kwa hivyo alikwenda na kujiegesha mtini pembeni ya mto, na sasa alifanya makusudi shoka lake litumbukie majini. Zebaki alitokea kama hapo awali, na, baada ya kujua kuwa shoka lake lilikuwa limeanguka, akazama na kuleta shoka la dhahabu, kama alivyofanya kwenye tukio lililopita. Bila kusubiri kuulizwa ikiwa ni lake au la yule mwenza alilia, "Hilo ni langu, hilo ni langu," na akanyosha mkono wake kwa hamu kuipata tuzo. Lakini Zebaki alichukizwa sana na kutokuwa kwake mwaminifu hivi kwamba si tu hakumpa shoka la dhahabu, lakini pia alikataa kumchukulia la kwake alililoliacha ianguke kwenye mto.

"Uaminifu ndio sera bora."

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno 30+ hapo chini kwa kuyazungushia na Penseli

J	Z	I	Z	Z	T	L	J	I	N	A	G	A	P	U	I	C	P	T
T	X	N	K	P	T	T	G	M	H	R	T	G	V	N	Z	I	C	J
B	I	I	J	M	M	C	N	N	A	H	N	A	I	M	H	N	L	N
R	S	B	U	A	Z	B	Q	R	K	J	A	B	W	I	N	L	Q	N
G	T	U	M	H	T	T	R	G	I	V	U	R	B	H	W	M	M	M
T	I	D	I	D	A	N	R	Y	N	R	L	N	I	Y	I	A	C	U
A	G	A	J	I	F	I	H	L	A	M	A	M	C	K	U	I	H	L
N	H	H	A	M	A	R	Z	D	K	T	U	M	A	L	H	R	D	A
Z	F	X	N	L	I	M	T	O	T	H	D	B	A	R	I	D	L	Q
I	A	C	U	X	H	N	M	W	T	A	I	N	I	N	K	G	A	A
A	R	B	J	L	D	M	T	T	H	O	A	L	A	B	W	A	D	T
Z	I	Z	A	W	A	D	N	A	T	U	K	B	A	A	A	P	Z	M
M	W	M	N	L	B	N	L	V	N	T	U	O	Q	F	N	T	U	I
T	F	V	L	H	L	O	M	F	R	H	S	F	K	N	A	A	B	Z
D	P	Z	I	R	A	A	T	K	U	A	E	J	X	I	D	T	B	N
I	S	I	D	N	A	H	M	R	L	E	Q	P	B	H	K	M	N	U
X	N	M	T	N	N	T	U	H	N	P	N	M	A	T	L	L	Z	R
K	C	M	R	N	H	F	K	X	V	C	R	M	P	N	Q	H	P	U
K	T	R	X	K	X	I	S	L	A	M	A	B	A	D	V	Y	F	K

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



Biskuti za Tangawizi

Na **Mtandao**







Vipimo

Unga - Vikombe 2
Cocoa ya unga - Kijiko cha supu
Sukari ya hudhurungi Kikombe 1
Siagi - ¾ Kikombe
Yai 1
Molasses - ¼ Kikombe
Baking soda - vijiko vya chai 2
Mdalasini wa unga - kijiko cha chai
Tangawizi mbichi - kijiko cha supu
Karafuu ya unga - ½ kijiko cha chai
Chumvi ½ kijiko cha chai
Vanilla ½ kijiko cha chai

Namna ya Kutayarisha na Kupika

Katika bakuli, chunga unga, baking soda, chumvi na cocoa. Weka kando. Washa oven lipate moto huku unatayarisha biskuti. Katika bakuli jengine, mimina siagi na sukari upige kwa mashini ya keki hadi mchanganyiko uwe laini kama dakika mbili. Mimina molasses na yai ndani ya mchanganyiko wa siagi na sukari uchanganye vizuri. Mimina unga kidogo kidogo huku unachanganya na mwiko hadi unga wote umalizike. Mimina mdalasini, karafuu na tangawizi, changanya vizuri. Weka mchanganyiko wako ndani ya jokofu kama masaa mawili. (*Ukipenda unaweza kuhifadhi mchanganyiko wako ndani ya mfuko wa jokofu gandishi na uoke siku nyengine.*) Tengeneza viduara vidogo vidogo.
Chovya kila kiduara katikati sukari, kisha panga kwenye treya ya kuoka. Rudisha viduara katika friji kama nusu saa. Oka katika 'oven' 350ºF kwa muda wa dakika 15. Toa biskuti kwenye oven na uache zipoe kama dakika kumi. Panga kwenye sahani tayari kuliwa.

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA AS

Umoja wa Mwenyezi Mungu

Umoja wa Mungu ni nuru iuangazao moyo baada ya kukatalia mbali miungu yote, iwe ni miungu ya dunia ya ndani au dunia ya nje. Huifunikiza kila chembe ya nafsi ya mtu. Hali hii yawezaje kupatikana bila msaada wa Mwenyezi Mungu na kumfuata Mtume Wake? Wajibu wa mtu ni kujiua nafsi yake na kuyapa kisogo majivuno ya kishetani. Asijigambe eti amelelewa kwenye kao la elimu, bali yuwapaswa kujihesabu kuwa mtu asiyejua cho chote, na kudumu katika maombi.
Ndipo nuru ya Umoja wa Mungu itamshukia na kumpatia maisha mapya.

(Roohani Khazain Jal. 22, Uk. 148: Hakikatul - Wahyi Uk. 144).

DARASA LA QUR'AN TUKUFU

Ahueni ya Hatari Zinazotuzunguka

Na **Musa Salum Mgeleka -** 0717 504 690

تَكَادُ ٱلسَّمَٰوَٰتُ يَتَفَطَّرۡنَ مِن فَوۡقِهِنَّۚ وَٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ يُسَبِّحُونَ بِحَمۡدِ رَبِّهِمۡ وَيَسۡتَغۡفِرُونَ لِمَن فِي ٱلۡأَرۡضِۗ أَلَآ إِنَّ ٱللَّهَ هُوَ ٱلۡغَفُورُ ٱلرَّحِيمُ

Ni karibu mbingu zipasuke toka juu yao, na Malaika hutukuza kwa kumsifu Mola wao na huwaombea msamaha waliomo ardhini. Angalieni! hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu, Mwenye huruma. Surat Ash-Shura: 6

MBINGU ni Paa 2:23 na Paa huangalia vyema athari mbaya za mazingira na kustawisha maendeleo mbalimbali. Mazingira yanaharibiwa basi Paa huharibika katika mazingira kama hayo ufanisi wa Paa huondoka. Manufaa ya mbingu huondoka na kusalia Fadhili na Rehema za Allah moja kwa moja. Rehema ya vitu vilivyofanywa Rehema inapoondoka, Rehema inayobakia ni Rehema ya Allah ya moja kwa moja isiyopitia kwa vitu. Rehema hii ni Kubwa na ndio hunusuri vitu vyote vinavyozungukwa na Hatari. Anguko, ajari, maafa, ugomvi, hitilafu hutokea ikiwa Rehema ya Allah ikikosekana.

Aya hii imeeleza namna tatu ambazo zikitumika au zinavyotumiwa huwezesha kuwepo kwa Nusura ya shida zote;

1. Kumtukuza kwa kumsifu Mwenyezi Mungu. Kumtukuza Allah kulimuokoa Nabii Yunus a.s asibaki kwenye tumbo la Samaki 37:140-144
2. Kuombea msamaha waliomo ardhini. Ndio njia ya Rehema 71:11-13
3. Mungu ni Msamehevu, Mwenye huruma. Ambao hawafanyi makosa hali wa wakijua 3:136-137 hali hii imeendelea kuinusuru dunia na watu wake. Makosa mengi ni ya ujinga au kusababishiwa hivyo huruma ya Allah huwakumba.

Mola wetu, Usitutwike tusiyoyaweza, na Utusamehe, na Utughofirie, na Uturehemu; Wewe ndiwe mlinzi wetu; basi Utusaidie juu ya watu makafiri. Amin

Sheikh Ibne Sheikh



Tungepeda kuwapasheni habari ya furaha kubwa ya kuwasili kwa tunda jingine la Jamia Ahmadiyya, Sheikh Ayaz Ahmad Dogar ambaye ni mwana wa Sheikh wetu mpendwa Sheikh Riaz Ahmad Dogar, Sheikh wa Mkoa wa Iringa. Sheikh Ayaz Ahmad Dogar alizaliwa mjini Rabwah Pakistan mnamo tarehe 7 Agosti 1991 na ni miongoni mwa Waqf-e-Nau (watoto ambao wazazi wao waliweza kuwatoa waqfu kabla ya kuzaliwa kwao kwa ajili ya kuitumikia Islam kwa agizo maalum la Khalifa Mtukufu wa Nne^{ra}). Sheikh Ayaz Ahmad alihitimu masomo yake ya shule ya msingi mjini Rabwah. Sheikh Ayaz alikuja Tanzania mnamo 2005 pamoja na wanafamilia wengine waliokuja kuungana na baba yao na kukaa huku kwa idhini ya Khalifa Mtukufu. Khalifa wetu mpendwa alipotutembelea mnamo 2005 basi Sheikh pia alipata bahati ya kuonana naye zaidi ya mara moja. Aliweza kukaa mjini Tabora kwa muda wa mwaka mmoja pamoja na baba yake kisha mjini Iringa kwani baba yake alihamishwa huko na Sheikh Ayaz alihitimu masomo yake yake ya sekondari akiwa mjini Iringa kisha alimaliza astashahada ya Sayansi ya Kompyuta na kwenda Jamia Ahmadiyya Ghana kwa idhini ya Khalifa Mtukufu mnamo Agosti 2014 na kuhitimu Jamia Ahmadiyya Ghana mnamo Aprili 2021 na kupata Shahada ya "Shahid". Yeye alikuwa miongoni mwa wanafunzi hodari katika masomo yake na kushika nafasi ya pili kwenye kila darasa. Tunamkaribisha Tanzania na kumpongeza sana kuja huko hasa kuchaguliwa kuwa mwalimu wa Jamia Ahmadiyya Tanzania. Mwenyezi Mungu Ambariki sana na kumpa uwezo maalum kwa ajili ya kuitumikia Islam Ahmadiyya. Amin

MATUKIO KATIKA PICHA



Sheikh wa Mkoa Shinyanga alishiriki mkutano maalum iliyoandaliwa na ofisi ya Mhe DC Shinyanga. Mgeni Rasmi alikuwa Mhe. Mkuu wa Mkoa na Katibu Twala pia alikuwepo. Viongozi wengine wa dini mbalimbali na serikali pia walishiriki hafla hii.



Sheikh wa Mkoa Dodoma alitembelea Mheshimiwa Mkuu wa wilaya.



Kambi ya Malezi Mbinga na Nyasa Zones



Amir Jamaat akihutubia Semina ya Malezi iliyoandaliwa na Majlis Ansarullah Dar es salaam



Sadr Khuddamul Ahmadiyya Tanzania, Rahim Mwanga sahib akiwatubia washiriki wa Ijtimaa ya 31 ya Khuddamul Ahmadiyya



Zoezi la upandishaji wa bendera katika ufunguzi wa Ijtimaa ya Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania



Wanajamaat wa Kahama, Shinyanga wakimlaki Amir na Mbashiri Mkuu alipowasili kwa ajili ya Jalsa Salana



Amir na Mbashiri Mkuu, Sh. Tahir Mahmood Chaudhry pamoja na Katibu Mkuu wa Ziada, Sh. Abdulrahman Ame wakiongea na waandishi wa habari juu ya Jalsa Salana ya Shinyanga

Vijana wa KiAhmadiyya wafanya Ijtimaa yao ya 31

Na **Ahmad Abdulrahim**
Add. Muhtamim Ishaat - MKA-TZ

Kutoka uk. 1

za taasisi zilizingira kauli mbiu hii kwa mwaka mzima. Mtaala wa mashindano ya kitaaluma chini ya kauli mbiu hii na michezo ulipelekwa mikoani miezi kadhaa kabla ya Ijtimaa na hivyo kuweka muda wa kutosha wa maandalizi.

Baada ya sala ya Ijumaa, washiriki wote walikusanyika katika ukumbi mkuu wa mkutano kusikiliza Hotuba ya Ijumaa iliyotolewa na Hazrat Khalifatul Masih V atba kisha kikao rasmi cha kwanza kikaanza kwa usomaji wa Quran Tukufu na tafsiri yake ikifuatiwa na shairi. Baadaye Khuddam na Atfal waliongozwa na Sadr Majlis katika kiapo cha Tanzim na zoezi la upandishaji bendera lilifuatia akiwepo mwakilishi wa Amir Jamaat katika ufunguzi wa Ijtimaa, Dokta Swaleh Kitabu Pazi sahib.

Kama kawaida, kulikuwa na mashindano anuwai ya kielimu na michezo kwa Khuddam na Atfal. Kulikuwa na mashindano ya soka ambayo yalianza Ijumaa jioni baada ya ufunguzi wa Ijtimaa kwa Khuddam, kuvuta kamba, riadha, mbio fupi. Khuddam na Atfal walifurahia sana mashindano, Alhamdulillah.

Jumamosi, baada ya Tahajjud, Fajr na Darsa la Quran Tukufu, mashindano ya kimwili yaliendelea na baada ya chai mashindano ya kielimu yalianza. Khuddam na Atfal walishindanishwa katika Hifdh-ul-Quran, tafsiri ya Quran Tukufu, hadithi za Mtume$^{s.a.w.}$, kuandika na kusoma hotuba, uandishi wa insha, kughani na kutunga mashairi, na mengineyo.

Mbali na mashindano, wahudhuriaji walipata fursa ya adhimu ya semina shirikishi ya maswali na majibu juu ya afya na njia za kujikinga na magonjwa iliyotolewa na dokta Mahmood Mwanga sahib na Ufafanuzi wa michango mbalimbali ya Tanzim na Jamaat iliyotolewa na Muhtami Mal, Abdallah Msesemel sahib. Pia Khuddam na Atfal walipata fursa ya kutambulishwiwa kundi la wasaidizi wa Mfalme wa Kalamu lijulikanalo kama majlis Ansar Sultanul Kalam na kufahamishwa madhumuni ya kuanzishwa kwake na kusisitiziwa uanachama hai ili kuitetea Islam juu ya mashambulizi ya maadui katika zama hizi za kalamu.

Kwenye kikao cha mwisho, bwana Seif Hassan Nakuchima, Katibu Mkuu wa Jumuiya alihudhuria Ijtimaa akimwakilisha Amir Jamaat ambaye alikuwa katika Jalsa za kanda ya ziwa na kuwahutubia Khuddam-ul-Ahmadiyya waliohudhuria na kutoa zawadi sambamba na Sadr Majlis kwa washindi wa mashindano mbalimbali.

Kwa fadhila za Allah na kupitia maombi ya Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba}, Ijtimaa ilikuwa ya mafanikio makubwa.

Kitengo cha Ishaat (machapisho) cha Majlis Khuddam-ul-Ahmadiyya kilitilia maanani sana kuitangaza Ijtimaa kupitia mitandao ya kijamii na gazeti hili. Matangazo yalisambazwa kabla ya Ijtimaa kuchajisha mahudhurio na mwisho wa Ijtimaa zilisambazwa picha za baada ya tukio.

Siku ya Khilafat Jamia Ahmadiyya

Na **Mwl Shamhuni Juma**

Kutoka uk. 1

Mgeni rasmi katika maadhimisho hayo alikuwa ni mkuu wa Chuo Cha Jamia Ahmadiyya-Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhatti sahib.



Wanafunzi wa Jamia Ahmadiyya Tanzania wakisikiliza mada zinazohudhurishwa kwao katika Siku ya Ukhalifa

Ikiwa chini ya mwenyekiti Maulana Sheikh Ahmad Daud sahib, hafla hiyo ilianza kwa usomaji wa Quran Tukufu iliyosomwa na Ustadh Idris Juma na kufuatiwa na shahiri la Ki- Urdu lililosomwa kwa pamoja na vijana watatu.

Baada ya shahiri hilo ilifuata hotuba iliyotolewa na Mwl. Shamun Juma,katika hotuba yake mwalimu alinukuu aya kadhaa na hadithi mbalimbali kuelezea umuhimu wa ukhalifa katika Islam na awamu mbili zab khilafat sawa na kauli ya Mtume Mtukufu (s.a.w) .Mwalimu pia alirejea matukio kadhaa yaliyotokea zama za makhalifa wote ,matukio ambayo yanasisimua na kujenga imani. Na mwisho mwalimu alinukuu sehemu ya nasaha za Hazrat Khalifatul-Masih III^{ra},ambaye alisema, "Ukhalifa udumu kati yenu daima na kila mwaminio wa silsila hii asimame imara kuulinda hata kama kwa kutoa dhabihu ya nafsi yake na maisha yake".

Baada ya hotuba hiyo,zilifuata nasaha za mgeni rasmi,ambaye alieleza wajibu na majukumu ya kila mwanajumuiya juu ya Ukhalifa. Alisema,ingawa ni jukumu la kila Mwaahmadiyya,lakini watumishi wa Jumuiya wana wajibu mara mbili zaidi kuliko wanajumuiya wa kawaida.Hivyo alitumia nafasi hiyo kuwakumbusha wanafunzi na waalimu wa Jamia wajibu wa kudumisha na kuimarisha Ukhalifa kuwa ni jukumu lililo mabegani mwao.

Mwisho mgeni rasmi aliongoza maombi ya kimya na kufunga mkutano.

Makhalifa Walioongoka - Hadhrat Umar ibn Al-Khattab^{ra}

Kutoka uk. 11

kutoka kwenye vinu hivyo unapaswa kupelekwa kwa Hadhrat A'ishah^{ra}. Hii ilionyesha heshima kubwa aliyokuwa nayo kwa wake na familia ya Mtukufu Mtume^{saw}. Wanawake wa Madina walikuwa hawajawahi kuona unga laini kama huo hapo kabla, na kwa hivyo wakakusanyika karibu na Hadhrat Bibi A'ishah^{ra} kuutazama. Khalifa wa Pili^{ra} alisema kwamba huu haukuwa unga maalum, bali ulikuwa wa kiwango kidogo kuliko unga ambao maskini kabisa walistahili kula. Wakati Hadhrat A'ishah^{ra} alipoweka unga uliopikwa kinywani mwake, alianza kulia. Alipoulizwa kwa nini alikuwa akilia, alisema alikuwa akimfikiria Mtukufu Mtume^{saw} ambaye hata katika siku zake za mwisho za maisha hakuwa na chakula cha kutosha. Mtu ambaye fadhila zote zilipatikana kwa sababu yake alikuwa amefariki, lakini wao waliweza kufaidika na fadhila na upendeleo huu. Baadaye Hadhrat A'ishah^{ra} alisema kuwa hawezi kula tena.

Khalifa mtukufu^{atba} alisema kwamba ataendelea kuangazia maisha ya Hadhrat Umar^{ra} katika hotuba za Ijumaa zijazo.

Mwishoni khalifa mtukufu^{atba} aliwataja baadhi ya wanajumuiya waliofariki hivi karibuni na kusema ataongoza Sala ya jeneza ya ghaib.

Miongoni mwa hawa waliofariki aliowataja yumo Bw. Issa Mwakitalima sahib, Naib Amir wa Jumuiya ya Tanzania. Khalifa mtukufu^{atba} alieleza historia yake kwa ufupi kwamba yeye awali alikuwa Mkristo. Kwa sababu ya tabia zake nzuri alipopata ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa^{as} hakuonesha ubishi na upinzani wa aina yoyote bali alikubali madai ya Seyyidna Ahmad^{as} na kujiunga mara moja na Jumuiya. Baadae mke wake pia akaungana naye kujiunga na Jamati.

Yeye alikuwa ni mtu mwenye tabia njema, alikuwa anaongoza katika utoaji wa michango kwa hiyo akawa katika swaf ya kwanza ya utoaji wa mali. Yeye alikuwa ni mtu mwenye khulka njema. Alikuwa anaonesha heshima na kuwajali wabashiri na viongozi wa ngazi zote za jamati kwa kuonesha ushirikiano nao mzuri. Yeye aliteuliwa kuwa raisi wa mkoa wa Dar es salaam, naye alikuwa ana upendo mkubwa na watu. Baadae akateuliwa kuwa Naib Ameer naye alikuwa anatoa mashauri mazuri kwa ajili ya ustawi wa jamati. Naye alikuwa anafanya kila juhudi ili nidhamu ya jamaat iwe imara na ya kudumu.Yeye alikuwa anajali sana mahitaji ya watu mbalimbali na kuyatekeleza. Yeye alitenga chumba kimoja katika nyumba yake ili iwe sehemu ya sala ya jamaa kwa ajili ya wanajumuiya katika eneo alilokuwa anaishi. Yeye alikuwa amefanya wasia.

Mwisho kabisa khalifa mtukufu^{atba} aliwaombea marehemu wote msamaha wa madhambi yao kwa Mwenyezi Mungu. (Amiin).

Kwa nini *Biblia Ni Jibu* Wanamkana Nabii Issa kuwa Si Yesu?

Na **Juma Iddy Abeid,** Kigoma

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

AKAJA KATIKA NASABA

Akasema akina Mariam wako wengi. Tatizo si kufanana majina tatizo ni Mariam yupi alimzaa Yesu na Mariam yupi hakumzaa Issa ?akasema kwa mujhibu wa kitabu cha Qurani Mariam alie mzaa Issa ni dada yake na Haruni .akanukuu sura ya 19:28- Ewe dada yake Hruni akanukuu sura ya mtu ambaye wala mama yake hakuwa hasherati

Ayah ii imeonesha jinsi watu walivyokuwa wakimshutum Mariamkwa ku mzaa motto ambae baba yake hajulikani

Hivyo kwa mjibu wa maandkop hayo Mariam ni dada wa Haruni ambaye ni ndugu yake na Musa mwisho waku nukuu

Mwandishi naye anaonesha naye anamjua Haruni mmoja tu duniani Halafua Qurani kunukuu shutma zawatu inakuwa ni tatizo la Qurani kunukuu shutums za watu inakuwa ni tatizo la Quraniyote iyo nikukosa uadilifu kwa mwandishi

Ukweli nikwamba nasaba mikitu kinacho kuwa na Mzunguko mrefu

Lakini hata uwe mrefu kama wa Matayo ambayo unafika kwa Adam . Ila vyeo ni vilevile tu Baba –Mama – Babu – Bibi –Mjomba - Shangazi dada- kaka –Mbwa – Binam uo ndio mzunguko yana sababu zinazo tuzunguka .Hivyo sio ajabu sana ila chamsingi nikurudi atika maeda yake ya Mariam kuwa dada yak e Harun Je Mariam yeye anajua ni dada ya wanani ?maana mtu kubisha usicho kijua mi ujinga usio na mwanga

Qurani inasema Mariam alipo pata mimba alienda sehemu za mbali 19:23 Je Mariam wa Biblia anasmuliwa vipi ?

LUKA 1:39 Basi Mariam akaondoka siku izo akaenda hata nchi ya mlimani kwa haraka mpaka mmoja wa Yuda kwa Eliza bati kabla ya miezi mitatu kisha rudi anakwenda nyumba ni kwake LUKA 1:56

JE Eliza bati na Mariam walikuwaje ni nasaba ?Bila shaa atakuwa anajua

Swali linguine je Eliza beti na Mariam walikuaje ni nasaba ?Bila sahaka atakuwa anajua .

Swali linguine je Elizabeti ni ukoo gani ?LUKA 1:5 zama za Herode mfalme wa Uyahudi palikuwa na kuwani mmoja jina lake ni Zakaria wa zama za Abiya na mkewe alikuwa mmoja wapo wa uzaao wa Harun jina lake Elizabeti kwa hoja iyo itakuwa vichekesho eti Mariam utakaa kwa mtu usie na undugu wowote kwa muda wa miezi mitatu mfululizo bila shaka ni mtu na ndugu yake pia Biblia inasema Elizabeti huyo ni mmoja wa uzao wa Haruni yupi .

Hivyo hapo qurani haviyumiwi kwa Qurani imenukuu masimuliza ya walio hoji juu ya Mariyam kuwa na Mimba ambayo walitilia mashaka na hao ndio waliokuwa kuwa wanajua uhusiano wa Mariam na Elizabati wapoje na Elizabeti na Haruni wapoje kwa kupima hicho inaonesha bado Mariam anae ongelewa na Qurani ndie huyo huyo anae ongelewa na Quran ndie huyo huyo anae ongelewa na Quran indie huyo huyo anae ongelewa na Quran indie huyo huyo anae anae ongelewa na luka mtakatifu wa kujitegemea Luka 1:1

Hivyo Qurani haikumwita Mariam kuwa dada wa Haruni ila Qurani imenukuu habari ya watu walio mshutumu Mariam kwa kuzaa nje ya utaratibu wanao ujuwa wa ndani ya ndoa kwani Qurani inajua kuwa Haruni alkuwepo katika zama za Mussa na Mariam huyo mama yake Yesu alikuwa ni mama wa Yesu aliezaliwa miaka1400 baada ya Haruni hivyo Qurani haiwezi kumwita hivyo lakini kwa mujibu huo wa luka unaonesha Mariam alikuwa na nduguye aitwae Haruni ndio kusema usipokijuwa kitu sio hakipo.

KUZALIWA KWAO

Mwandishi ataanza na kumnukuu Issa ndani ya Qurani katika Sura 19:23 Basi akabeba mimba akaondoka nae mpaka mahali pa mbali

19:24; kisha uchungu ukampeleka mpaka penyeshana la mtende (akawa anazaa huku anasema)kiti nina kufa mara ukimfikia sauti kutoa chini yake (inamwambia) usihuzunike hakika mola wako amejaliwa (amewake) kajito cha maji chini yako na litikise kwako shina la mtende Alipo Maliza kunukuu akanzaaa vichekesho badala ya hoja eti aya ni maaelezo yaliyo ndani kitabu cha Qurani ambayo yanaeleza kwa undani jinsi Issa alivyozaliwa kwa mujibu wa maelezo hayo nikuwa Baada ya maongezia kati ya Malaika jibril na Mariam akawa tayari mja mzito na akawa na anza Muda huohuo hiyo ndio Qurani juu juu ya kuzaliwa Issa

Lakini ni tofauti ya kuzaliwa Bwana Yesu . maana tukisoma kitabu cha Luka 2:11-12-Maana tukisoma Maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa kwa jili yenu mwokozi ndie kristo Bwana nahii ndio Ishara kwenu mtakuta motto mchanga amevaa nguo yakitoto amelala katikati ya hori ya Ng'ombe kwa maandiko ayo Issa ni Mwungine Yesu ni mwingine mwisho wa kunukuu. Ukweli jamaa hawa wa Biblia ni jibu wana jaribu kuonesha tofauti ambayo ili mradi ziwatenganishe kati ya Issa na Yesu . Lakini haiwezekani labda kwa uelewa finyu wa uchambuzi wa Maandiko lakini ukitizama utakuta Kurani ilizingumzia Yesu alipozaliwa na Biblia imeongelea alipo lazwa baada ya kuzaliwa baada ya kuzaliwa Issa alipelekwa wapi kuhifadhiwa vivyo hivyo. Biblia Imetaja alipo ifadhiwa akiwa kaisha safishwa na kuvikwa nepi na sweta . Lakini haitaji Mariam alipo patia uchungu wa uzazi wala alipo zaliwa hivyo hoja hivyo inakupa yenyewe.

Ila ajabu Zaidi inayo tia mashaka ni Luka 2:4 ambapo panasema Yusufu alienda katika mji wa wa kwao ili alesabiwa yeye na Mariyam.

Ajabu mtu mwenyewe kwao akakuta nyumba za wageni zimejaa .Halafu huo mji wa kwao hakakosa hata Shangazi wa kumuhifadhi.na kumua kujihifadhi zizini.

Itaendelea toleo lijalo

Makhalifa Walioongoka - Hadhrat Umar ibn Al-Khattab ra

Kutoka uk.12

haionekani siku hizi, imeenda wapi? Yeye akajibu ukali wangu ulikuwa unatumika mahala pasipostahili lakini sasa unatumika katika mahala pake sahihi.

Baada ya kifo cha hadhrat Abu Bakar ra na baada ya hadhrat Umar ra kuwa Khalifa alisimama mbele ya masahaba kuwahutubia. Kwanza aliomba dua kwa Mwenyezi Mungu kuwa: Ee Mola wangu mimi ni mtu niliye dhaifu, Unijaalie nguvu kutoka kwako. Mimi ni mtu mwenye tabia ya ukali, Unijaalie ulaini. Mimi ni mtu bakhili, Unijaalie kuwa mkwasi. Kisha akawahutubia watu akiwaambia enyi ndugu zangu; Mwenyezi Mungu Ametupa mtihani kwa mimi kuwa Khalifa kwenu na ninyi kuwa wafuasi wangu na wale watangulizi wangu wawili (mtume saw na Abu Bakar ra) wamekwishafariki kabla yangu. Mwenyezi Mungu Ameniteua mimi kubaki pamoja nanyi. Basi yale mashauri yenu mtakayoyaleta kwangu mimi ndiye nitakaye husika nayo, ima yale mambo yatakayotokea sehemu iliyokuwa mbali na mimi nitamkabidhi mtu mwingine mwaminifu ili ayashughulikie. Kama watu wataonesha ushirikiano mzuri na nidhamu ya ukhalifa sisi pia tutalipa kwa mambo mazuri kwao, lakini kama wataasi sisi tutawalipizia sawa na vitendo vyao.

Khalifa mtukufu atba alisema kuwa siku ya tatu baada ya kuwa Khalifa, Hadhrat Umar ra alitoa hotuba ambayo alisema kwamba alikuwa amesikia watu wanaogopa hasira yake kali na kwamba watu waliona atakuwa mkali kama kiongozi.

hadhrat Umar ra alisema kuwa atakuwa mkarimu sana, lakini wakati huo huo atakuwa thabiti katika kuhakikisha kuwa haki inatekelezwa kila wakati.

Khalifa mtukufu atba alisema kuwa Khalifa wa Pili, Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad ra alisema kuhusu Khilafat ya hadhrat Umar ra, kwamba alijitahidi sana kuhakikisha kwamba maadili na mafundisho ya Uislamu yanazingatiwa. Hadhrat Umar ra alikuwa akimwomba Mwenyezi Mungu, kwamba amekabidhiwa jukumu kubwa, na anaomba maghfira ikiwa hatatenda haki katika kutekeleza jukumu hili.

Hadhrat Muslih Maud ra anasema waandishi wa magharibi ni watu wa ajabu, linapokuja suala la mtume saw wao wanaonesha upinzani na kumlaumu vikali. Lakini linapokuja suala la uongozi wakati wa ukhalifa wa hadhrat Umar ra wanatoa sifa kubwa kuwa haujapata kuwepo uongozi ulio nzuri kama ule wa Umar ra, ambapo maisha yote ya Umar ra yamepita katika malezi ya mtume saw. Hivyo jambo hili linawezekanaje, mlezi awe ni mtu mbaya na mlelewa wake awe ni mtu mzuri. Basi maana yake ni kwamba waandishi wa magharibi hawako tayari kukubali kuwa mtume saw alikuwa ni mtu bora kwa sababu ya husda na bughudha yao dhidi ya mtume saw.

Khalifa mtukufu atba alisema wakati Iran iliposhindwa, vinu vya kusagia unga vililetwa Madina, na Hadhrat Umar ra alisema kuwa unga wa kwanza

Endelea uk 10

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

SHAW.-DH.QAD 1442 AH | JUNI 2021 | IHSAN 1400 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufusaw

"Mtume*saw* alikuwa anasema, "Pengine unalazimika kutoa sadaka, lakini hutoi, basi haramu inaangamiza mali yako ya halali. Bila shaka haramu haichanganyiki na halali ila inaihilikisha." (**Kashf-ul-Gumah**)

Makhalifa Walioongoka - Hadhrat Umar ibn Al-Khattab*ra*

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 18/06/2021; Baada ya Tashahhud, Ta'awwudh na Surat Faatihah, Khalifa Mtukufu V, Hazrat Amir ul Momeniin, Mirza Masroor Ahmad*atba* ('Ayyadahullahu Ta'ala Bi-Nasrihil Aziiz') alisema; Pindi wakati wa kifo cha Hadhrat Abu Bakar*ra* ulipokaribia, akamwita Abdulrahman bin Auf*ra* kupata ushauri wa jinsi Umar*ra* alivyo naye akajibu Umar*ra* ni mzuri zaidi kuliko vile unavyofikiria, lakini ndani yake kuna ukali kidogo. Hadhrat Abu Bakar*ra* akajibu ukali wake ni kwa sababu ya ulaini wangu. Kwani katika baadhi ya maswala ambamo mimi ninakuwa laini yeye anakuwa mkali na katika maswala yale ambamo mimi ninakuwa mkali yeye anakuwa laini.

Kisha hadhrat Abu Bakar*ra* akataka ushauri kutoka kwa hadhrat Uthman*ra*. Yeye akasema undani wake ni mzuri zaidi kuliko hali ya nje yake. Baadae hadhrat Abu Bakar*ra* akawaambia wote wawili ushauri niliopata kutoka kwenu msimwambie mtu yeyote.

Imekuja katika simulizi moja kuwa sahaba mmoja alifika kwa hadhrat Abu Bakar*ra* akamwambia ewe Amirul muminuun! Tumesikia kuwa wewe unataka



*Masjid Mubarak: Hadhrat Khalifatul Masih V*atba *huhutubia Ijumaa kwa waaminio tokea na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.*

kumteua Umar awe khalifa wetu baada yako, lakini wewe unajua fika kuwa yeye ni mkali kwetu kiasi gani. Hadhrat Abu Bakar*ra* akajibu pindi nikatakapokuwa mbele ya Mwenyezi Mungu nitamwambia mimi nimemteua mtu aliye bora katika watumishi wako wote kuwa Khalifa baada yangu mimi.

Katika riwaya nyingine imekuja kuwa pindi wakati wa kifo cha hadhrat Abu Bakar*ra* ulipokuwa unakaribia alimwita hadhrat Uthman*ra* kumwandikisha wasia. Wakati wa kuandika wasia huo mara hadhrat Abu Bakar*ra* akapoteza fahamu, ndipo hadhrat Uthman*ra* alipoandika jina la hadhrat Umar*ra* katika wasia huo kuwa khalifa baada ya hadhrat Abu Bakar*ra*. Alipozinduka na kupata fahamu tena hadhrat Abu Bakar*ra* akamwambia soma tena ule wasia tuliokuwa tumeandika. Hadhrat Uthman*ra* akasoma wasia wote ambamo liliandikwa jina la hadhrat Umar*ra*.

Baada ya kusikia hayo hadhrat Abu Bakar*ra* akasema wewe umeandika wasia sahihi na hata kama ungeandika jina lako katika wasia huo pia ungekuwa umepatia kwani wewe pia unastahili kuwa Khalifa. Ndipo hadhrat Abu Bakar*ra* akawaita masahaba wote na kuwahutubia kuwa mimi nimemteua Umar*ra* kuwa khalifa wenu baada yangu mimi na akaongeza kuwa mimi sijamteua ndugu yangu yeyote wa damu kuwa khalifa wenu baada yangu mimi. Kisha akawauliza watu wote, je, mnakubaliana na maamuzi yangu haya. Wakajibu tumesikia nasi tunatii.

Imekuja tena katika riwaya nyingine kuwa hadhrat Abu Bakar*ra* akamwita hadhrat Umar*ra* naye akamwusia ucha-mungu. Akamwabia bila shaka umeshaona kuwa zile aya zenye kuusia mambo ya ulaini zimekuja na aya zinazousia tabia ya ukali kidogo na zile zenye ukali zimekuja na aya zenye kuusia mambo ya ulaini kidogo ili katika mwaminio kuwe na uwiyano wa ukali na ulaini. Kwa hiyo mimi nakuusia ucha-mungu katika maswala yako wewe mwenyewe na katika maswala ya wale utakaowaongoza.

Hahdrat Khalifatul Masih 1*ra* anasema baadhi ya watu wakamwuliza hadhrat Umar*ra* mbona ile tabia yako ya ukali

Endelea uk 11



KITABU

Haja ya Imamu

Kitabu hiki, ambacho kimeandikwa na Hadhrat MIrza Ghulam Ahmad wa Qadian, ambaye amedai kuwa Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi, aliyesubiriwa na dini zote kuu za dénia, kinarekodi shuhuda mbili za kiungu kuunga mkono madai yake.

Shuhuda zilitolewa na watakatifu wawili wa Kiislam kwa majina Gulab Shah na Nei'matullah Wali ambao waliishi muda mrefu kabla yake na walishuhudia ukweli wake katika mwanga wa funuo za kiroho walizopokea.

Hivyo, kitabu kinaangazia umuhimu wa shuhuda za kimbingu kwa dunia kumjua na kumtambua Imam na mteule wa kiroho wa zama. Kikiandikwa chini ya ufunuo wa kiungu, kitabu kitatia mvuto kwa wale ambao hutafuta mlinzi halisi wa ujumbe wa kiroho katika kila zama na wakati.

Jipatie nakala yako kwa bei ya maktaba ya Tsh· 3,000/=

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com